HABARI
**SERIKALI YAAHIDI UMEME WA UHAKIKA**
Uk.5



**Mpango wa kuimarisha huduma za afya Tanzania, Ufaransa waiva**
Uk. 4



AZIMIO LA NISHATI BORA DAR ES SALAAM LILIVYOFANIKIWA
Uk.5

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2518 JUMANNE FEBRUARI 04, 2024 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# DODOMA HAPATOSHI MIAKA 48 YA CCM

>> **Dkt.** Samia, Dkt. Mwinyi Dkt. Nchimbi kutambulishwa kwa wana CCM

>> **Bodaboda,** Bajaji kunogesha Jiji la Dodoma

>> **Dodoma** yote kupambwa na Kijani na njano

>> **Ni** dalili tosha ya ushindi wa kimbunga Oktoba

Uk.2




*Picha katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini ambayo Kitaifa yamefanyika katika viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma, jana ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan.*

## Dkt. Biteko aonya uwepo Makundi ndani ya CCM

Uk.2



# DODOMA HAPATOSHI MIAKA 48 YA CCM

NA MWANDISHI WETU

CHAMA Cha Mapinduzi CCM, kimetangaza rasmi kuwa wagombea wake wa Urais kupitia chama hicho watatambulishwa katika kilele cha sherehe za miaka 48 ya chama hicho zitakazofanyika jijini Dodoma.

Wagombea hao ni pamoja na Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan anayegombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwingine ni Dkt Huusein Ali Mwinyi atakayepeperusha bendera ya CCM kugombea Urais wa Zanzibar.

Akizungumza na Waandishi wa Habari jijini Dodoma Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, CPA. Amos Makalla alisema vilevile Mgombea Mwenza wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Emmanuel Nchimbi naye atatambulishwa katika sherehe hizo.

Makalla amemtaja mgeni rasmi kuwa ni Dkt Samia huku akiwaalika wanachama wa CCM na wananchi kuhudhuria sherehe hizo ambazo zinatarajiwa kufana kama ulivyofanyika Mkutano Mkuu wa CCM Januauri 18 na 19 jijini humo.

Alisema maaandalizi ya mkutano huo yanaendelea kukamilika, ambao pia utahudhuriwa na viongozi mbalimbali wa CCM pamoja na marafiki wa chama hicho.

"Hizi ni sherehe za CCM, hivyo siku hiyo tutawatambulisha wagombea wetu kwa wana CCM lakini siku ikifika tutawatambulisha kwa wananchi."

Makalla alisema CCM kinatimiza miaka 48 kikiwa ni chama imara kilichoaminiwa kushika dola kikiwa na wanachama 12 milioni hivyo kina dhamana na heshima kubwa.



# BITEKO AONYA UWEPO WA MAKUNDI NDANI YA CCM

NA MWANDISHI WETU

WAKATI Chama Cha Mapinduzi CCM kikijiandaa kufanya sherehe za maadhimisho ya miaka 48 Jumatano ijayo jijini Dodoma naye Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Dkt. Doto Biteko ameonya uwepo wa makundi ndani ya chama hicho kuelekea uchaguzi badala yake nguvu kubwa ielekezwe kwenye kujenga umoja na kutowapa nafasi wapinzani.

Dkt. Biteko amesema hayo katika mkutano wa Jimbo la Chamwino ulioendana na uwasilishaji wa utekelezaji wa ilani ya CCM katika kipindi cha maka mitano ya mbunge wa Jimbo hilo, Deogratius Ndejembi ambayo pia n Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

"Uchaguzi unaokuja ni uchaguzi usiokuwa wa majaribio ni uchaguzI unaotaka kungana kwa pamoja na tulivyo wengi, tunaweza tukawa na tofauti mbalimbali na misimamo ya aina tofauti niwaombe tuache tofauti zetu tukitazame chama tushikamane kwa pamoja hatuna sababu ya kuhangaika kuwazungumza wengine tuzungumze mambo tuliyonayo ndani ya chama chetu," alisema Dkt. Doto Biteko.

Aidha Dkt. Biteko aliongeza kuwa "Nchi yetu ina vyama vingi vya siasa vina kazi mbili na chama kimoja kina kazi ya kufanya na chama kingine kina kazi ya kusema nyie wana CCM fanyeni kazi, hivyo vyama vingine viachieni maneno ya kusema wananchi watawapima kwa kazi sio kwa ma-

# SERIKALI YAAHIDI UMEME WA UHAKIKA

NA MWANDISHI WETU

MATATIZO ya kukatika umeme yaliyokithiri katika maeneo mengi ya nchi yanaendelea kupatiwa ufumbuzi na serikali, ili kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kwa uhakika.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga ambaye aliahidi serikali inahakikisha wananchi wanapata umeme wa uhakika na kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Kapinga aliyasema hayo jana Januari 03, 2025 Bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la la Mbunge wa Lushoto Mhe. Shabani Shekilindi aliyetaka kufahamu ni lini Serikali itaondoa changamoto ya kukatika umeme katika Wilaya ya Lushoto kwa kuweka suluhisho la kudumu.

Alisema serikali itafuatilia kwa kipindi cha wiki moja ili kufahamu ni jambo gani linasababisha changamoto ya kukatika kwa umeme wilayani Lushoto.

"Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge iwapo kuna matengenezo tutahakikisha yanakamilika kwa haraka," alisisitiza Mhe. Kapinga

Akijibu swali Mbunge wa Nkasi Kusini, Mhe. Vicent Mbogo aliyetaka kufahamu uwepo wa nishati ya umeme katika Kijiji cha Msamba-Masokolo, Lyapinda, Izinga na Lyele na katika Vitongoji vya Kisenga na Lupata, Mhe. Kapinga amesema Wilaya ya Nkasi ina jumla ya vijiji 90 ambavyo vyote vimepatiwa huduma ya umeme vikiwemo vijiji vya Lyele na Lyapinda.

Aidha, amesema Kitongoji cha Lupata kilichopo katika Kijiji cha Lyapinda kitapata umeme kupitia mradi wa Vitongoji 15 vya Mbunge utakaotekelezwa na Mkandarasi aitwae M/s STEG International Services Ltd ambaye ameshakamilisha hatua za upimaji na usanifu.

NAIBU Waziri wa Nishati Judith Kapinga, amesema kwamba changamoto ya mgao wa umeme nchini itaisha rasmi mwezi wa Machi, mara baada ya mtambo namba 9 wenye uwezo wa kuzalisha megawati 235 kufanyiwa majaribio jana na mwingine utajaribiwa mwezi wa ujao, hali ambayo itaondoa adha ya umeme nchini.

Kauli hiyo aliitoa, Bungeni baada ya kuulizwa swali na Spika wa Bunge Dkt Tulia Ackson kwamba ni lini mgao wa umeme utamalizika katika taifa hili.

"Tuliahidi mwezi huu tuna ratiba ya kuzindua mtambo huu (mtambo no 9 katika mradi wa Bwawa la Julius Nyerere) na ratiba hii iko palepale, tunawashukuru sana

Watanzania kwa kuendelea kutuvumilia, matumizi ya umeme yanategemeana tukizalisha mwezi huu mgao utakuwa umepungua kwa kiasi kikubwa kwa sababu tunazalisha megawati 235 na mwezi wa tatu tutazalisha megawati 235 hivyo zitakuwa megawati 470 uhakika ni kwamba kufikia mwezi wa tatu mgao wa umeme utaisha nchini,"

# Umoja wa vijana kuanza shereha za CCM mapema

NA MWANDISHI WETU

CHAMA cha Mapinduzi ( CCM ), kinatarajia kufanya sherehe kubwa za kudhimisha miaka 48, zitakazofanyika Tarehe 5 Februari 2025 katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma ambapo Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Kuelekea Maadhimisho hayo, Jumuiya ya Umoja wa Vijana (UVCCM) imejipanga kuanza shamrashamra hizo kwa kualika Vijana wote katika mbio za Marathon ya 48 pamoja na tamasha, vyote vikifanyika tarehe 4 katika ukumbi wa Jakaya Convention Centre.

Marathon hiyo itafanyika February 04,2025 ambapo Vijana wataanza mbio kuanzia Jakaya Kikwete Convention Centre kuanzia saa 12:00 asubuhi ikifuatiwa na burudani kutoka kwa Wasanii mbalimbali.

Maadhimisho haya yanakwenda kufanyika ikiwa ni siku chache zimepita toka Chama hicho kieleze kuwa kwa sasa kina Wafuasi zaidi ya milioni kumi na mbili ( 12,000,000).



# SERIKALI KUIMARISHA JESHI LA ZIMAMOTO



NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa amesema kuwa Serikali inaendelea kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vitendea kazi ambapo sasa inatekeleza mradi wa ununuzi vifaa mbalimbali vya kuzima moto na uokoaji pamoja na magari 150 ya kuzima moto na uokoaji.

Bashungwa ameeleza hayo tarehe 03 Februari 2025 wakati akijibu swali la Mbunge wa Ngorongoro, Emmanuel Shangai aliyetaka kujua Je, lini Serikali itanunua gari la Zimamoto Wilaya ya Ngorongoro.

"Kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa ununuzi vifaa mbalimbali vya kuzima moto na uokoaji pamoja na magari 150 ya kuzima moto na uokoaji" amesema Bashungwa

Amesema pindi magari 150 ya kuzima moto na uokoaji yatakapofika nchini, yatakayosambazwa nchi nzima ikiwemo Wilaya ya Ngorongoro.

Aidha, amesema Serikali inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshaliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kununua magari 12 ya kisasa ambapo moja wapo lilitumiaka kuzima moto katika jengo gorofa la TRA Kariakoo.

Bashungwa amesema Serikali ipo mbioni kununua helikopta moja maalum kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambayo yataenda sambamba na kuwapatia Mafunzo Maafisa, Wakaguzi na Askari wa Jeshi hilo.

# Azimio la nishati bora Dar es Salaam lilivyofanikiwa

NA MWANDISHI WETU




VIONGOZI wa nchi na serikali za Afrika waliafikiana na kuunda Azimio la Dar es Salaam yaani 'Dar es Salaam Energy Declaration' lililolenga kuhakikisha upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

Maafikiano hayo yalifikiwa katika Mkutano wa Nishati wa 'Mission 300 'ulifanyika kwa siku mbili nchini Tanzania, ukihudhuriwa na wakuu wa nchi 24 za Afrika, Mawaziri wa Nishati na Fedha, pamoja na viongozi wa Taasisi za kifedha na nishati za kimataifa, ambapo jumla ya viongozi 2,600 walishiriki.

Azimio la Dar es Salaam limepewa kipaumbele kama hatua muhimu ya kushughulikia changamoto kubwa za nishati zinazozuia maendeleo ya bara la Afrika.

Miongoni mwa mambo mengine yaliyomo kwenye azimio hili ni kila nchi kushiriki katika kugharamia upatikanaji wa umeme na kuimarisha uwezo wa utekelezaji wa miradi ya umeme kwa wakati.

Azimio linasisitiza usawa wa kijinsia katika kuongeza upatikanaji wa nishati, hasa kwa wanawake na wafanyakazi, ili kuimarisha mustakabali wa nishati endelevu.

Pia azimio linatoa msisitizo mkubwa kuhusu umuhimu wa kuunganisha nishati kati ya nchi za Afrika, kutumia vyanzo vya nishati jadidifu kama vile jua, upepo, umeme wa maji, nishati ya joto la ardhi, na mchanganyiko wa nishati ili kuwa na mifumo imara ya nishati.

Viongozi hao pia walihimiza ushiriki mkubwa wa sekta binafsi, ubunifu, na kuweka mazingira bora ya kisheria ili kuhamasisha maendeleo, kuboresha miundombinu na kufanikisha mageuzi ya nishati kote Afrika.

Waunda Tume ya kufuatilia masuala ya umeme Afrika

Kwa kuongezea, siku ya jana viongozi hao walikubaliana kuanzisha Tume ya Umoja wa Afrika itakayoratibu na kufuatilia utekelezaji wa azimio hilo, kwa lengo la kutokomeza tatizo la umeme na kuimarisha uchumi katika nchi za Afrika.

Aidha, watahakikisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia, kutumia nishati mbadala, na kupunguza madhara ya uharibifu wa mazingira.

Viongozi hao pia walikubaliana kuongeza ufanisi wa miundombinu ya uzalishaji, upitishaji, na usambazaji wa nishati kwa gharama shindani, huku wakifanya kazi pamoja katika kukuza mifumo ya ununuzi shindani na wazi.

Sekta binafsi kubeba ukuaji nishati Afrika

Wakuu hao wa nchi walikubaliana kuvutia mitaji kutoka sekta binafsi na kuhakikisha fedha zinazohitajika kwa ajili ya miradi ya mabadiliko ya nishati zinapatikana.

Azimio hili pia linatoa wito wa utekelezaji wa mipango wiliyoafikiwa ikiwa na malengo ya muda mrefu ya kupata fedha kwa ajili ya miradi ya nishati safi.

Sehemu ya azimio hilo linasema: "Lengo letu ni kufikia watu milioni 300, na tunapendekeza hatua madhubuti na ushirikiano wa kisiasa katika utekelezaji wake. Tunaomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuwezesha utekelezaji wa azimio hili."



# MPANGO WA KUIMARISHA HUDUMA ZA AFYA TANZANIA, UFARANSA WAIVA

NA MWANDISHI WETU

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya Dkt Seif Shekalaghe hivi karibuni alishiriki katika hafla ya utiaji saini hati ya makubaliano kati ya Serikali ya Ufaransa na Hospitali ya Aga Khan kuhusu uimarishaji wa huduma za saratani katika Hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam.

Katika hafla hiyo iliyofanyika hospitali ya Aga Khan, Serikali ya Ufaransa iliwakilishwa na Balozi wake nchini Mhe. Anne Sophie Av'e, ambaye ameeleza hisia zake kuhusu namna ugonjwa huo unavyoathiri wanawake nchini na kusababisha changamoto katika familia.

Hati hiyo ya makubaliano imesainiwa baada ya wa awali ambao ulidumu kwa miaka minne kumalizika muda wake.



Hata hivyo amefurahishwa kwa uanzishwaji wa kituo cha matibabu ya Saratani katika Hospitali ya Saratani ya Ocean Road ambacho ni tumaini kwa akina mama wengi wenye matatizo ya Saratani.

Akitoa salamu za Wizara ya Afya katika halfa hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. Seif Shekalaghe ameishukuru Serikali ya Ufaransa kwa msaada inayoutoa kwa Hospitali ya Aga Khan na kwa Tanzania kwa ujumla na ameahidi Serikali kuendelea kushirikiana na hospitali hiyo katika kuhakikisha mradi huo unafanikiwa.

Aidha, Katibu Mkuu ameitaka Hospitali ya Aga Khan pamoja huduma inazozitoa kwa wananchi ni vema pia kusaidia katika kuwajengea uwezo watumishi wa afya ili waweze kubaini dalili za saratani mapema na kutoa matatibu mapema au rufaa, kushirikisha jamii katika kutoa elimu kuhusu saratani ili waweze kufika vituoni mapema na kufanyiwa vipimo.

Pia ametaja maeneo mengine kuwa ni kusaidia utafiti katika eneo la saratani ili kubaini sababu za changamoto kwa lengo la kuwa na majawabu ya kudumu na ushirikiano kati yake na taasisi za Serikali ili kuimarisha ubora wa huduma kwa wagonjwa wa Saratani.

Dkt Seif Shekalaghe amesema kwamba kuhudhuria kwake katika hafla hiyo ya kusaini hati ya Makubaliano ni ishara kuwa Serikali ipo tayari kushirikiana na wadau wa sekta ya afya katika kuimarisha huduma za afya ikiwemo za Saratani.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# ACT Walalendo yaibuka msimamo wa Trump




NA MWANDISHI WETU

CHAMA Cha Siasa ACT Wazalendo kimeguswa na uamuzi wa Serikali ya Marekani kusitisha kwa muda kwa mikopo na ruzuku za kusaidia huduma za afya Duniani, hatua inayoweza kuathiri mamilioni ya Watanzania waliowekwa kwenye utegemezi wa huduma za afya zinazofadhiliwa na mashirika ya nje.

Tanzania, kama moja ya wanufaika wakubwa wa misaada ya hiyo kutoka Marekani kupitia Shirika la Misaada ya Marekani (USAID), Mpango wa dharura wa Rais wa Marekani wa kupambana na UKIMWI (PEPFAR), Mfuko wa Dunia (Global Fund), Mpango wa Kupambana na Malaria (PMI) imechangia kwa kiasi kikubwa katika mapambano dhidi ya magonjwa kama UKIMWI, kifua kikuu, malaria, na huduma za chanjo kwa watoto.

Kwa Mfano, hadi kufikia Machi 2024, Tanzania ilikadiriwa kuwa na watu milioni 1.7 wanaoishi na VVU, ambapo zaidi ya milioni 1.5 wanatumia dawa za kufubaza makali ya UKIMWI (ARVs) tunazotegemea kutoka nje.

Mapema mwaka huu Global Fund ilitangaza ufadhili wa dola za Marekani milioni 602. Sawa na Shilingi trilioni 1.57 kwa matibabu endelevu ya waathirika wa VVU.

Aidha, ACT Wazalendo kupitia Baraza Kivuli la Mawaziri tumekuwa tukiionya Serikali kuhusu utegemezi huu wa kifedha kutoka nje kwenye kutoa huduma za afya, ambapo unaweka rehana maisha ya watanzania. Takriban 41% ya bajeti ya afya ya Tanzania inategemea Mashirika ya misaada ya kimataifa, tena kwa huduma za magonjwa hatari zaidi.

Kwa miongo mitatu, Serikali ya CCM imekuwa ikiacha suala la afya kwenye mabega ya wananchi wenyewe au wafadhili kutoka nje. Bajeti ya afya ya Tanzania ni chini ya asilimia 5 ya bajeti kuu ya Serikali, kinyume na makubaliano ya Abuja yanayotaka kutengwa kwa asilimia 15 ya bajeti kuu kwa ajili ya sekta ya afya.

Hivyo, uamuzi huu utaivua nguo Serikali kwa kuweka wazi makosa yake ya kutoweka kipaumbele kwa afya na kuweka maisha ya Watanzania kwenye mikono ya wafadhili wa kigeni.

ACT Wazalendo, hatutaki makosa ya Serikali ya CCM yasiwaangamize watanzania, tunaitaka Serikali ichukue hatua zifuatazo;

Serikali ipunguze matumizi yasiyo ya lazima na kuelekeza fedha kwenye huduma za afya zinazotishiwa na kusitishwa kwa misaada ya nje.

Kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya ya Kitaifa kwa kutumia rasilimali za ndani kama madini na utalii kufadhili mfumo wa afya unaojitegemea.

Serikali iongeze bajeti ya afya kutoka wastani wa asilimia 5.7 hadi kufikia 10% ya bajeti kuu 2025/2026, ili kupunguza utegemezi na kuboresha huduma ya afya.

Serikali iharakishe utekelezaji wa mfumo wa kuwaunganisha watanzania na Hifadhi ya Jamii na kutoa bima ya afya kwa wote ili kuongeza uwezo wa serikali kugharamia na kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma za afya bila ubaguzi wa kifedha.

ACT Wazalendo tunasisitiza kuwa ni wajibu wa Serikali ni kuhakikisha inatumia rasilimali vizuri ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wote kwa usawa, si kwa kutegemea wafadhili wa nje. Serikali haipaswi kufanya mambo ya anasa huku ikiwaacha wanachi wake wanaishi kwa kutegemea hisani.

# TAHARIRI

## Kwa hili CCM inastahili pongezi

WANACHAMA wa Chama Mapinduzi (CCM), sambamba na wananchi wote Tanzania wametakiwa kuwa makini na viongozi wenye tabia ya uchonganishi kwa kile walichodai baadhi yao kuchochea chuki inayoweza kuwatenganisha.

Hiyo ni kauli makini iliyotolewa na katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa ndugu Amos Makalla wakati akizungumza na Wananchi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi katika Viwanja vya Umoja ni nguvu kusini Pemba ikiwa ni muendelezo wa ziara yake ya Mikoa 6 Visiwani Zanzibar.

Makalla pia amesema kuwa Dkt Samia Suluhu Hassan na Dkt Hussein Mwinyi hawana ubaguzi wowote kwenye suala la kuwaletea maendeleo lakini wenzetu kila kukicha wanaweka fitina na hili kazi kwenu Wazinzabar kwa ujumla wakataeni Viongozi hao na wanasiasa hao kwa kuwanyima kura wakati Uchaguzi utakapofika na tuchague chama cha mapinduzi ambacho ndio kina wajibu wa kuyaleta.

Kauli hii haistahili kupita bila kupongezwa ndiyo maama sisi JAMVI LA HABARI tunaipongeza kwa vile imezingatia kuleta umoja mshikamano na maelewano baina ya Watanzania.

Tunasema hayo tukijua kwamba kipindi kijacho yani Mwezi Oktona nchi itaingia katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na Madiwani hivyo wasioitakia mema nchi wanaweza kutumia nafasi hiyo kuingiza chuki na hasama baina ya wananchi.

Tunaamini kila aliyesikia rai hii iliyotolewa na chama tawala, atazingatia kwa vile nchi hii ina wanasiasa na wasio wanasiasa ambao wanahitaji amani na utulivu.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778, - 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684, - 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz





*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (katikati) akiwa katika mkutano na waandishi wa Habari kuelezea Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2025.*

UCHAMBUZI

# Ushindi wa CCM unatokana na utekelezaji wa ilani yake

NA MWANDISHI WETU

SIRI kubwa ya maandalizi ya CCM Kushinda uchaguzi Mkuu na kuendelea kushika Doila, ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ambayo viongozi, waliopewa nafasi waliibeba na kuifanyia kazi kila eneo.

Hilo ndilo linaloweza kuwafanya wagombea wa chama hicho akiwemo mgombea nafasi ya Urais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na jopo la wviongozi wengine watakaopambania nafasi za Ubunge na Madiwani.

Tayari chama hicho kimefanya chaguzi za ndani kama vile ule uliohusisha Mkutano Mkuu wa CCM, ulimchagua Mzee Steven wassira kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara.

Wassura aliyekuwa nje ya madaraka ya kisiasa kwa muda mrefu kwa maneno yake mwenyewe alieleza kushangazwa na ushindi ule na akaahidi kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu na unyenyekevu mkubwa, kama hatua ya kulipa fadhjila na heshima ile kubwa.

Pia mkongwe huyo akatabiri ushindi wa kishindo utakaokipata chama chake, mtaji mkubwa ukiwa ni utekelezaji wa Ilani na jinsi chama hicho kinavyoendesha siasa zake kwa njia ya uwazi na uwajibikaji.

Mkongwe huyo ameingia na Falsafa ya Umoja Maridhiano na Ushindi, kazi ambayo amewaahidi wajumbe waliomuamini kushika wadhifa huo kuwa ataifanya kwa bidii kubwa huku akiamini ni jukumu lenye baraka za Mungu.

Kwa tathmini nyepesi ya ushindi huu wa Wasira una maana kubwa kwa CCM kuekelea uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka huu, mwezi Okttoba kwamba mtaji wake unaonekana umeongezeka

Ukichukulia kuwa CCM ndicho chama kinachoongoza nchini kwa kuwa na wanachama na wapenzi wengi kinaweza kutumia mtaji huo kumpa ushindi wa kishindo mgombea wake wa Urais na hata Wabunge na Madiwani.

CCM ina watu wengi hata isipohitaji kura ya wapinzani au watu wasiofungamana na siasa ya chama chochote bado wana uhakika wa kushinda hususa nafasi ya Urais pengine baadhi ya wabunge wachache wanaweza kupoteza viti kutokana na kutowafanyia vizuri wapiga kura wao katika kipindi kilichopita.

Mgombea wa CCM anasaidiwa na maendeleo yanayoonekana kila kona, atahitaji timu ya kawaida tu kumnadi na kuweza kumpa ushindi wa kimbunga kama huu alioanza kuonyesha dalili Mzee Wasira

Ushindi wa CCM mwaka huu unaonekana bila kuhitaji utafiti mkubwa, kwani hata ukiangalia upande wa upinzani bado unaonekana kama hakuna chama chenye nguvu kama ilivyokuwa katika chaguzi za awamu zilizoipita tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1992

Licha ya CCM kujiandaa kama ilivyokuwa wakati wote inapoingia katika uchaguzi, lakini mwaka huu licha ya uwepo wa maridhiano ya kisiasa, lakini upinzani unaonekana kupoteza nguvu kuliko miaka yote ya uchaguzi.

Ni mwaka tutakaoendelea kusikia vishindo vya CCM katika majimbo na makelele ya wapinzani watakaoendeleza msamiati wa kuibiwa kura ili hali hawakuwa na maandalizi zaidi ya malumbano na kukashifiana.

# CCM YATOA TAHADHARI K

NA MWANDISHI WETU

WANACHAMA wa Chama Mapinduzi (CCM), sambamba na wananchi wote Tanzania wametakiwa kuwa makini na viongozi wenye tabia ya uchonganishi kwani wanaweza kuchochea chuki inayoweza kuwatenga Watanzania.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa ndugu Amos Makalla wakati akizungumza na Wananchi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi katika Viwanja vya Umoja ni nguvu kusini Pemba ikiwa ni muendelezo wa ziara yake ya Mikoa 6 Visiwani Zanzibar.

"Sisi CCM tutetembee kifua mbele kazi ya kuwahudumia Wananchi wale wenzetu ni watu wa vituko ,uongo, fitina na majungu ndo kazi yao sisi tunajukumu na dhamana ya kuwaletea Wananchi maendeleo.

"Nayasema ivi kwasababu wanakuja hapa wanasema mnajenga maghorofa wakati watu wanakufa na njaa na miradi yote sio maendeleo sasa ndo ujue kuna shida na anaetamka hayo ni mtu mzima ndo mana nasema kazi ni kusema uongo na vituko lakini hawo hawo Viongozi ndugu zao wanasoma katika hayo maghorofa na wanapata huduma mbalimbali lakini hawazioni niseme muda wa kudanganyana umeisha pamoja majukumu walilojipa tuwaogope Viongozi fitina"

Mwenezi Makalla ameendelea kusema kuwa Dkt Samia Suluhu Hassan na Dkt Hussein Mwinyi hawana ubaguzi wowote kwenye suala la kuwaletea maendeleo lakini wenzetu kila kukicha wanaweka fitina na hili kazi kwenu Wazinzabar kwa ujumla wakataeni Viongozi hao na wanasiasa hao kwa kuwanyima kura wakati Uchaguzi utakapofika na tuchague chama cha mapinduzi ambacho ndo kina wajibu wa kuyaleta.

Wakati hayo yakiendelea kutoka Mwanza inaelezwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilemela Mhe Dkt Angeline Mabula ametatua mgogoro wa ardhi uliodumu kwa zaidi ya miaka 15 katika mtaa wa Kangaye kata ya Nyakato wilayani Ilemela uliokuwa ukihusisha wananchi wa mtaa huo na mwekezaji



Hassan Issa Shekila ni Mwenyekiti wa jumuiya ya wazazi ya chama cha mapinduzi kata ya Nyakato ambapo amemshukuru Mbunge wa Jimbo la Ilemela Mhe Dkt Angeline Mabula kwa juhudi zake katika kumaliza mgogoro huo na kufanikisha zoezi la upimaji kwaajili ya kumilikisha wananchi viwanja vyao baada ya kuishi maisha ya wasi wasi kwa muda mrefu

'.. Kiukweli tunampongeza Mbunge wetu, ni msikivu na amekuwa na Sisi kwa kipindi chote cha mgogoro huu, Kila tulipomuendea alitusikiliza na mara ya mwisho alikuja katika eneo lenye mgogoro na kutoa maelekezo yaliyosaidia Leo tuweze kupimiwa viwanja vyetu ..' Alisema

Aidha Ndugu Shekila amewataka wananchi wenzake kukumbuka fadhila za Mbunge huyo na kuhakikisha wanaendelea kushirikiana nae na kumuombea kwa Mungu Ili aweze kusimamia na kutekeleza shughuli za maendeleo za kila siku akishirikiana na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan

Nae Afisa upimaji wa ardhi manispaa ya Ilemela Ndugu Chacha Samson amefafanua kuwa yeye akishirikiana na wataalam wengine wanaendesha zoezi la kubaini mipaka na kupima eneo la mtaa wa Kangaye kata ya Nyakato ili kubaini vipande vya ardhi vya kila mwananchi ili mpango wa matumizi bora ya ardhi uweze kufuatwa na baadae wananchi wanaohusika waweze kumilikishwa viwanja hivyo

Kwa upande wake Bi Nu
ra Yahya Ramadhan amb
ni miongoni mwa wakazi w
eneo hilo wanaokabiliwa
mgogoro huo wa ardhi a
emshukuru Mbunge wa Jim
la Ilemela kwa kujitoa na k
hakikisha anashirikiana
Serikali kusaidia wananchi h
ambapo alifanya mikutano
hadhara na kuagiza wataala
wa manispaa ya Ilemela k
maliza mara moja mgogo
huo kwa kushirikisha ofisi ya

Manispaa ya Ilemela ilikuw
ikikabiliwa na migogoro mb

# KUEPUKA UCHONGANISHI




> Rais Dkt Samia Suluhu Hassan na Mbunge Dkt Angeline Mabula migogoro hiyo imeweza kupata ufumbuzi na kutatuliwa huku migogoro michache baina ya wananchi kwa wananchi






imbali ya ardhi ikiwemo uwanja wa ndege na wananchi wa kata ya Shibula, polisi Kigoto na wananchi wa kata ya Kirumba, Magereza na wananchi wa Ilalila, jeshi la wananachi na wananchi wa Lukube na mpaka sasa chini ya uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan na Mbunge Dkt Angeline Mabula migogoro hiyo imeweza kupata ufumbuzi na kutatuliwa huku migogoro michache baina ya wananchi kwa wananchi ikiendelea kumalizwa kwa asilimia kubwa.

# Mkutano Jukwaa la Korosho kufanyika Tanzania



NA MWANDISHI WETU

TANZANIA inatarajiwa kuwa mwenyeji katika Mkutano wa 19 wa mwaka wa Jukwaa la Korosho Afrika ambao kufanyika Novemba 18 hadi 22, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo umendaliwa na Jukwaa la Korosho Afrika (ACA) kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania na Umoja wa Wabanguaji Wakubwa wa Korosho Tanzania (TACP).

Pia Mkutano wa 19 wa Mwaka wa ACA unakusudiwa kuhudhuriwa na washiriki wasiopungua 500 kutoka nchi zote Duniani zikiwemo nchi 33 zinazolima korosho.

Baadhi ya nchi hizo ni pamoja na Ivory Coast, Cambodia, India, Vietnam, Brazil, Indonesia, Sri Lanka, Nigeria, Guinea Bissau, Burkina Faso, Mali, Benin, Ghana, Madagascar, Zambia, Msumbiji, Kenya, Mauritius, Visiwa vya Komoro na wenyeji Tanzania.

Akizungumza na Waandishi wa habari Januari 31, 2025 Jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Korosho Tanzania , Francis Alfred amesema Mkutano huo unakusudia kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko kwenye tasnia ya Korosho kuanzia shambani ambapo wanategemea kupata uwekezaji kwenye mashamba makubwa ya korosho, kuongeza ubanguaji ambapo matarajio ni kuongezeka kwa viwanda vya kubangua na kusindika korosho na bidhaa zake na kuimarika kwa masoko kwa kufungua masoko ya korosho na bidhaa zake ndani na nje ya nchi za Afrika.

> "Kwa mfano katika msimu wa 2024/2025 ruzuku ya pembejeo ilikuwa shilingi billioni 182. Utoaji wa pembejeo za ruzuku umechagiza kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 310,000 msimu wa 2023/2024

"Kwa upekee Mkutano huu utatumika kuhamasisha matumizi ya korosho na bidhaa zake kama vile mafuta ya ganda la korosho (Cashewnut Shell Liquid - CNSL), sharubati (juice), maziwa ya korosho (cashew milk), mvinyo (wine), nyama ya mabibo (cashew apple meat) na pombe kali. Aidha bidhaa nyingine kama ethanol zinaweza kutumika kwenye maabara za hospitali na shule zetu na hivyo kupanua wigo wa soko la korosho". Amesema Alfred.

Amesema mkutano huo utashirikisha wadau mbalimbali kutoka nchi ambazo ni walaji wa korosho ikiwa ni pamoja na Marekani, Nchi za Ulaya, China, Uarabuni, Mashariki ya Kati ikiwa ni pamoja na Afrika Kusini na nchi zingine za bara la Afrika.

Aidha amesema Serikali imefanya juhudi kubwa za kuendeleza zao la korosho ambapo kwa kipindi cha miaka mitatu sasa imekuwa ikitoa pembejeo za korosho kwa wakulima kwa ruzuku ya 100%.

"Kwa mfano katika msimu wa 2024/2025 ruzuku ya pembejeo ilikuwa shilingi billioni 182. Utoaji wa pembejeo za ruzuku umechagiza kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 310,000 msimu wa 2023/2024 hadi kufikia tani 410,000 kwa msimu wa 2024/2025 zilizouzwa kupitia minada". Amesema

Pamoja na hayo amesema ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji unaendelea kwa kukusanya takwimu za korosho zinazobanguliwa majumbani kwenye vikundi vidogo na watu binafsi pamoja na uzalishaji katika mikoa mipya.

Amesema hadi mwisho wa msimu makadirio ni kuzalisha jumla ya tani 500,000 katika msimu wa 2024/2025.

"Bei ya korosho ghafi katika msimu wa 2024/2025 iliimarika na kufikia shilingi 4,195 kwa kilo ikiwa ni bei ya juu kuliko bei zote zilizopatikana kutoka nchi yetu ipate uhuru.". Ameeleza Alfred.

Hata hivyo amesema pamoja na uwepo wa mahitaji makubwa ya korosho ghafi katika soko la dunia, uamuzi wa Serikali kutumia mfumo wa mauzo wa Soko la Bidhaa (TMX) umesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza ushindani katika minada na kuchangia katika kuimarika kwa bei.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa ACA, Ernest Mintah amesema Mkutano huo unatarajiwa kuwa na washiriki zaidi ya 400 kutoka nchi mbalimbali duniani ambapo hii itakuwa mara ya tatu kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huukwani mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka sita, baada ya kuwa mwenyeji wa mkutano huo mwaka 2008 na 2019.

Amesema Mkutano wa ACA umekuwa ukijikita kwenye mada kuu inayoundwa kupitia mchakato wa kina ili kuakisi hali halisi na kushughulikia changamoto kuu zinazoikabili sekta ya karanga duniani ambapo katika Mkutano huu itajikita zaidi na kauli mbiu ya "Kufungua Fursa za Uwekezaji katika Karanga kwa Ukuaji Endelevu wa Uchumi."

"Mkutano wa mwaka huu utaangazia hitaji muhimu la kuwekeza kimkakati katika maeneo kama vile utafiti, maendeleo ya uwezo wa binadamu, miongozo ya sera, ubunifu na teknolojia, ufuatiliaji, usalama wa chakula, na mengineyo katika sekta ya karanga ili kuhamasisha ukuaji endelevu". Amesema Mintah.

Nae Mwenyekiti wa Umoja wa wabanguaji wa Korosho, Bahati Mayoma amesema ili kuweza kushiriki kwenye mkutano wa 19 wa mwaka wa ACA kila mshiriki atatakiwa kulipia kiasi cha shilingi 400,000 kwa watakaojisajili na kulipia kabla ya tarehe 15 Oktoba 2025 na shilingi 500,000 kwa watakaojisajili na kulipia baada ya tarehe 15 Oktoba 2025 kwa watanzania .

Aidha kwa wageni amesema itakuwa nia dola za Marekani 500 kwa wanachama wa ACA na dola za Marekani 700 kwa wasio wanachama wa ACA kwa watakaojisajili na na kulipia kabla ya tarehe 13 Agosti 2025 na dola za Marekani 700 kwa wanachama wa ACA na dola za Marekani 1,000 kwa wasio wanachama wa ACA kwa wakakaojisajili na kulipia baada ya tarehe 31 Agosti 2025.

# UJUMBE MZITO WATUMWA DRC KUANGALIA USALAMA

NA MWANDISHI WETU



MKUTANO wa dharura wa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika umeagiza kutumwa mara moja kwa Mawaziri wa ulinzi na wakuu wa ulinzi kwa nchi zinazochangia wanajeshi nchini DRC, ili kuhakikisha wanajeshi wa ujumbe wa SADC katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (SAMIDRC) wako salama na kuwezesha kuwarejesha nyumbani mara moja wanajeshi waliofariki na wale waliojeruhiwa.

Hilo ni moja ya maazimio yaliyomo katika taarifa ya pamoja iliyotolewa baada ya kikao kilichofanyika Harare, Zimbabwe hapo Ijumaa ili kujadili hali mapigano makali huko mashariki mwa DRC kati ya wapiganaji wa kundi la waasi wa M23 wanaodaiwa kusaidiwa na Rwanda na vikosi vya jeshi la DRC kiasi cha waasi kuudhibiti mji wa Goma makamo makuu ya jimbo la Kivu Kaskazini. Mara kadhaa Rwanda imekuwa ikikanusha madai hayo.

Viongozi hao licha ya kutofafanua kuhusu ujumbe wa mawaziri wa Ulinzi na wakuu wa majeshi, wametoa salamu za rambirambi kwa DRC, Malawi, Afrika Kusini, na Tanzania kuhusiana na wanajeshi waliopoteza maisha katika mashambulizi ya hivi karibuni huko Sake, Mashariki mwa DRC, wakiwa chini ya SAMIDRC, na kuwaombea uponaji wa haraka waliojeruhiwa.

Taarifa ilifafanua kuwa wakuu hao wa nchi walipokea ripoti za karibuni zaidi kuhusu hali ya usalama inayoendelea mashariki mwa DRC na kubainisha masikitiko kuhusu mashambulizi ya hivi karibuni ya kundi la M23 na Jeshi la Ulinzi la Rwanda (RDF) dhidi ya vikosi vya Serikali ya DRC, ujumbe wa SADC katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (SAMIDRC), na raia katika maeneo mbalimbali ya Kivu Kaskazini.

Mkutano huo ulieleza kusikitishwa na hali kwamba mashambulizi ya hivi karibuni yameendelea kuzorotesha hali ya usalama na kibinadamu nchini DRC na kutaka kurejeshwa mara moja kwa huduma muhimu kama vile maji, umeme, njia za mawasiliano na njia za usambazaji wa chakula na bidhaa nyingine muhimu.

Mkutano huo umelaani vikali mashambulizi dhidi ya wanajeshi wa SAMIDRC yaliyofanywa na M23 wanaoendesha shughuli zao Mashariki mwa DRC kwani vitendo hivyo vilikiuka usitishaji mapigano uliosimamiwa na mchakato wa Luanda tarehe Julai 30, 2024 na kudhoofisha amani na usalama wa DRC na eneo la SADC.

Viongozi hao walikumbusha uamuzi wake wa Mei 2023 wa kupeleka ujumbe wa kulinda amani nchini DRC ili kuunga mkono matakwa yake ya amani na usalama na kulinda uadilifu wa eneo lake. Katika suala hili, Mkutano huo ulibainisha kuwa malengo haya bado hayajafikiwa.

Mkutano huo ulisisitiza kuunga mkono juhudi za kidiplomasia za kupata suluhu la amani kwa mzozo wa Mashariki mwa DRC kupitia mchakato wa Luanda, unaoongozwa na João Lourenço, Rais wa Angola na mtetezi mkubwa wa Umoja wa Afrika wa amani na maridhiano barani Afrika na mchakato wa Nairobi, ukiongozwa na Rais wa zamani wa Kenya, Uhuru Kenyatta.

Pia ulitolewa wito wa kufanyika kwa Mkutano wa haraka wa pamoja wa wakuu wa nchi za SADC na wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ili kujadiliana kuhusu hali ya usalama nchini DRC kama ilivyopendekezwa na mkutano wa 24 wa wakuu wa nchi za Jumuiya hiyo wa Januari 29, 2025.

Mkutano huo wa kilele umeipa mamlaka Troika, ambacho ni chombo cha SADC kuhusu siasa, ulinzi na ushirikiano wa usalama, kushirikisha pande zote za serikali na zisizo za kiserikali kwenye mzozo, kuhusu mchakato wa kusitisha mapigano ili kulinda Maisha ya watu na kuwezesha mtiririko mzuri wa misaada ya kibinadamu kwa watu na jamii zilizoathiriwa na vita.

Kikao hicho kiliwahimiza viongozi wa kisiasa na kidiplomasia ambao ni wahusika katika mzozo huo kushiriki katika juhudi zilizoratibiwa za mazungumzo, ikiwa ni pamoja na kuunga mkono mchakato wa Luanda, MONUSCO na wengineo, ili kurejesha amani na usalama Mashariki mwa DRC.

# MAENDELEO YA NCHI NI KETE YA TURUFU KWA DKT SAMIA KATIKA UCHAGUZI MKUU

NA MWANDISHI WETU

MARA nyingi utaratibu wa vyama kufanya kampeni katika zoezi la uchaguzi, ni jambo la kikatiba, lakini wakati mwingine kiongozi akitimiza majukumu yake suala hili la kampeni linakuwa rahisi pia.

Utawala wa CCM Awamu ya Sita chini yake Rais Dkt Samia Suluhu Hassan umekuwa ni wenye mafanikio makubwa kutokana na kutimiza Ilani ya Uchaguzi ya Chama hicho, hii ikionekana ni karata muhimu kwa mgombea huyo wa nafasi ya Urais na hata chama chake.

Hivi sasa Wabunge watakaosimama kupitia tiketi ya CCM hawakuwa na kazi kubwa ya kujieleza kushawishi wananchi kuwapigia kura kutokana na kazi kubwa ya maendeleo inayoonekana iliyofanywa na serikali hii.

Anastahili kuwa Rais aliyefanikiwa katika kizazi hiki, maana ukiangalia maboresho na hatua aliyopiga kuyakimbilia maendeleo unaweza kukiri kwamba amepanda zaidi ule mzani kwani hakuna awamu unayoweza kuinasibisha, bali inabaki kuwa na msemo wa kila zama na historia yake.

Mara nyingi ninapoandika makala nikielezea hali ilivyokuwa enzi za utawala wa Awamu ya Kwanza chini ya Uongozi wa hayati Mwalimu Julisu Nyerere, wananibana katika hoja ya mafanikio.

Kwamba je? baada ya hayo yaliyokuwa yakiimbwa kila kona na kunadiwa katika maadiko na hata kukaririwa na wanafunzi wa ngazi tofauti, mafanikio yake yalikuwaje?

Kwangu si maswali ya msingi, maana yanakwenda kwenye masuala ya utekelezaji, mafanikio au kushindwa, maeneo ambayo yapo nje ya hoja zangu.

Kiu ya Makala hii ni kuweke 'Jicho Kongwe' katima vichwa Chipukizi vya vijana wa leo, ambao ndiyo asilimia kubwa ya Watanzania kwasasa, wapate ufahamu juu ya kule tulikotoka na huku twendako!

Lakini huwa siweki shaka hata robo kuwa nitakuwa Majununi kama nitathibutu kuyafananisha maendeleo, mfano yale ya awamu ya kwanza na hii ya sita maana kila kitu kinapishana kwa hatua kubwa.

Siyo mantiki yangu kuorodhesha yale yaliyofanikiwa katika utawala wowote wa nchi hii, iwe Awamu ya Kwanza hadi ya Sita, Watakwimu mimi siyo miungoni mwao.

Japokuwa ukiniuliza mafanikio yasiyohitaji tathmini au kuingia kwenye 'Vijaruba' vya watunza kumbukumbu nitakujibu kuwa ni "Mama anaupiga mwingi' na ukitaka

***Tuendelee kushukuru kwa kila hatua, mengi ya Awamu wa Sita yanatufumbua macho, kuona yale tuliyohisi kiasili yanapaswa kuonekana Ulaya tu, leo Afrika na hususan Tanzania tunazungumza sauti moja na wale wanaosihi Texas.***



mifano nitakutembeza na kukuonyesha Reli ya Kisasa, Nitakupeleka ukaone maendeleo kule Bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere na maeneo mengine ambayo huko awali nisingepata fursa hiyi

Lakini ukiuliza siri ya urithi wa utulivu wa Taifa nitarudi kwenye vitabu na kukumbusha jinsi Mwamu Nyerere alivyotuunganisha kwea kupinga ukabila na Udini

Huu mseto wa makabila mfano Mzanaki kuzaa na Mpemba, Mmakonde kupata mke katika familia ya Wanyiramba, haikuwa kazi nyepesi, juhudi hizi ndiyo mafanikio tunayoyanadi kuwa ni mafanikio ya Utawala wa Mwalimu Julius Nyerere.

Ukiacha eneo hilo pia tunaangalia jinsi Watanzania walivyoshiriki kwa nguvu zote kupigana vita dhidi ya maadui watatu wa Taifa, Ujinga, Umasikini na Maradhi.

Maadui hawa watatu hata kama waliisumbua jamii ya Watanzania toka nchi ilipopata Uhuru Tarehe 9 Desemba 1961 hadi hhivi sasa, lakini enzi hizo kila Mtanzania mwenye akili timamu, alifahamu jukumu lake la kupambana na maadui hawa.

Hii ilitokana na Somo la Uzalendo jinsi lilivyowaiingia Watanzania na msingi wake ulijengwa katika elimu iliyokuwa ikitolewa, tangu kwa wanafunzi wa masomo ya awali hadi vyuoni, swali la kuwajua Maadui Watatu wa Taifa halikuhitaji mwanafunzi afike darasa fulani, hata anayesoma chekechea aliweza kuwataja bila ya kumeza mate.

Hii ilisaidia jamii ya kujifunza uzalendo na kukataa kuishi katika mambo yanayotajwa kama ni miiko ya Taifa, mfano Kutoa au Kupokea Rushwa, kutumia cheao kwa faida ya mtu binafsi, na mengine yaliyokuwa katika nukuu za Ahadi 10 za Mwana TANU, Watanzania waliyabeba kama mzigo wao.

Leo hii ukiukwaji mkubwa wa haki za Binadamu, ukosefu Maadili, kutochukia Rushwa na Ufisadi ni mazao ya vijana wetu walioamua kuyapa kisogo, masomo ya uzalendo.

Ni wale wanaopata vyeo na kutohisi kuwa Tanzania ni ya kila mwananchi na rasilimali hizi zipo kwa ajili ya kizazi hiki, kulingana na mahitaji ya kihistoria ya uzawa!

Tunaweza kukiri kuwa tumechelewa, lakini bado tuna nafasi ya kufika, kwani miguu yetu ingalipo safarini.

Tuendelee kushukuru kwa kila hatua, mengi ya Awamu wa Sita yanatufumbua macho, kuona yale tuliyohisi kiasili yanapaswa kuonekana Ulaya tu, leo Afrika na hususan Tanzania tunazungumza sauti moja na wale wanaosihi Texas.

Akikwambia kuwa alipanda Treni la Umeme kutoka Texsan kwenda Miami hutoshangaa ilivyokuwa kwani na wewe unamiliki usafiri huo katika nchi yako.

Aliyewahi kuona awamu zote za nchi hii hawezi kumaliza maneno bila kumuombeas dua huyu Mama aliyeshika kijiti Awamu ya Sita kwani maneno kwake yamekuiwa machache zaidi ya vitendo. Mungu Ibariki Tanzania.



# MIKOANI NI DKT SAMIA, DKT MWINYI NA CCM 2025

NA MWANDISHI WETU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoani hapa kimeunga mkono uamuzi wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kuwapitisha Dkt Samia Suluhu Hassan, Dkt Hussein Mwinyi na Dkt Nchimbi kuwa wagombea Urais kupitia CCM mwaka huu.

Pongezi hizo zimetolewa na Viongozi mbalimbali wa chama hicho kwenye maandamano ya amani yaliyofanyika juzi mjini hapa ambapo walieleza kuwa hatua hiyo imetokana na kasi na weledi mkubwa walioonesha katika utendaji wao.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora Said Mkumba amesema kuwa wamefanya maandamano hayo ili kuunga mkono uamuzi huo kwa kuwa viongozi hao 2 wameonesha uwezo mkubwa na kusimamia kwa asilimia 100utekelezaji ilani.

ëUamuzi huo ni ishara tosha kwamba wanaCCM tumeridhishwa na uwezo wao na kasi yao ya kusimamia utekelezaji ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa asilimia 100 na tuna imani kubwa kwaoí, ameeleza.

Amebainisha kuwa uamuzi huo unamaanisha kwamba Rais Samia na Mgombea mwenza Dkt Nchimbi ndio chaguo la wanaCCM kwenye urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Mwinyi kwenye urais wa Zanzibar.

Nkumba ameeleza kuwa kasi ya maendeleo yaliyoletwa na Rais Samia na Rais Mwinyi kule Zanzibar ni kielelezo tosha kuwa Viongozi hawa wanatosha kupewa mitano tena na huo ndio uamuzi wa mwisho wa wanaCCM wote.

ëRais Samia ni mwanamke shujaa na kiongozi makini mwenye maono makubwa ya kimaendeleo, tumepokea uteuzi huo kwa mikono miwili, Tabora tunaunga mkono mapendekezo hayo kwa asilimia 100í, amesema.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mohamed Nassoro amesema kuwa CCM ni chama imara na kitaendelea kuchagua Viongozi makini, wazalendo, wachapa kazi, wanaojali watu na siyo maslahi binafsi na wenye kauli safi.

Amebainisha kuwa Rais Samia, Rais Mwinyi na Emanuel Nchimbi ni chaguo sahihi, wana kila sifa zinazotakiwa na watanzania wote na wameonesha uwezo mkubwa katika utendaji wao.

ëWatanzania wana kila sababu ya kuwashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa maamuzi hayo ambayo yatawapa nafasi wagombea hao wa CCM kujipanga vizuri kwa ajili ya uchaguzi mkuu utakaohusisha vyama vya upinzanií, amesema.

Naye Katibu wa CCM Mkoa Wilson Nkambaku ameeleza kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wameonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa na katiba ya chama inawapa nafasi ya kuendelea kushika nafasi hiyo.

Amebainisha kuwa wapinzani hawajawa na uwezo wa kuongoza nchi, hivyo akawataka kuendelea kujifunza kwa Chama Cha Mapinduzi hadi watakapokuwa na uwezo wa kujisimamia huku akiongeza kuwa serikali ya CCM itaendelea kuwaletea maendeleo wananchi pasipo kujali itikadi zao.

Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, amesoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020/2024, akisema ameitekeleza kwa asilimia 100.

Taarifa hiyo aliwasilisha leo Januari 24, 2025, mbele ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Jimbo la Shinyanga Mjini, ambapo Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, Ally Hapi, alikuwa mgeni rasmi.

Katambi, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), amebainisha mafanikio katika sekta mbalimbali, ikiwemo elimu, afya, miundombinu, maji, na nishati safi ya kupikia.

Elimu

Mbunge Katambi amesema ndani ya miaka minne, shule mpya tisa zimejengwa, zikiwemo shule za msingi tano na sekondari nne. Aidha, alifanikiwa kuanzisha tawi la Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na kupanua Chuo Kikuu cha Moshi (KICoB) tawi la Kizumbi.

Miundombinu

Katambi ameeleza kuwa miundombinu ya barabara, madaraja, na masoko imeboreshwa. Alitaja ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Ibadakuli, daraja la Uzogole, na maboresho ya barabara katika maeneo ya Iwelyangula, Ibinzamata, Ndala, Ihapa, Mwamalili, na Mwanoni.

Afya

Ameboresha huduma za afya kwa kujenga vituo vya afya, zahanati sita, na hospitali, ikiwemo Kituo cha Afya Kambarage na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga. Pia, alitoa ambulensi sita kwa msaada wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Maji

Amesema mtandao wa maji umeongezwa katika maeneo ya Bugwandege, Masekelo, Mwamasheke, Mwanubi, Busongo, na maeneo ya mjini. Zaidi ya shilingi bilioni 195 zimetengwa kwa usambazaji wa maji kwa kipindi cha 2024/2025.

Mikopo na Ajira

Ameeleza kuwa shilingi milioni 200 zilitolewa kwa vikundi vya Boda boda, Bajaji, wanawake, na watu wenye ulemavu kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Pia, milioni 19 zilipatikana kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.

Nishati Safi

Katambi amegawa mitungi ya gesi 1,780 kwa makundi mbalimbali ili kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Michezo

Mbunge huyo alianzisha ligi mbalimbali za michezo, ikiwemo utoaji wa zawadi za hadi shilingi milioni 6 kwa washindi wa mashindano.

Katambi amewataka wana-CCM kushirikiana kwa ajili ya maendeleo na kuepuka migogoro. Aliwasihi viongozi wa chama kuendelea kushirikiana kwa manufaa ya wananchi.

Katibu wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Odilia Batimayo, amempongeza Katambi kwa kazi nzuri na alionya dhidi ya kampeni za mapema za kugombea ubunge. Ally Hapi naye alimsifu Katambi kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM, akisema mafanikio hayo yanaongeza imani ya wananchi kwa chama.

Hapi amewataka wagombea kuzingatia maadili ya chama, kujiepusha na wapambe wa kisiasa, na kuendeleza siasa za kisayansi kwa kujenga hoja kwa wananchi.

Katika hafla hiyo, Katambi pia amekabidhi kiti mwendo kwa mtoto mwenye ulemavu, Delfina Mashaka, na vifaa vya sauti kwa uongozi wa Stendi ya Mabasi ya Mkoa wa Shinyanga.



# Michezo Kimataifa



## JOSEPH KANIKI 'GOLOTA' MPACHIKA MABAO ALUYEACHA HISTORISA SIMBA

NA HENRY PAUL

UKIWAULIZA wanachama na mashabiki wa Simba, kuwa miaka ya 2000 mwanzoni ni mpachikaji mabao gani wa timu yao aliyekuwa na mashuti makali, ni dhairi watakuambia kuwa ni Joseph Kaniki au 'Golota' kama mashabiki hao wa Kariakoo, mtaa wa Msimbazi walivyozoea kumwita.

Mpachikaji mabao huyo aliyekuwa na mwili mkubwa wa kimichezo, alikuwa na kila kitu ambacho mshambuliaji mahiri anatakiwa kuwa navyo, ambavyo si uwezo mkubwa wa kupachika mabao pekee, bali pia mashuti makali na kutumia nguvu pale inapohitajika.

Mkongwe huyo pamoja na kuanza kujulikana kidogo akiwa na timu za mitaani huko Mburahati, lakini umaarufu mkubwa alianza kuupata alipojiunga na Simba mwaka 2000.


Wakati alipojiunga na Simba, miongoni mwa wachezaji aliowakuta na kucheza nao ni Mohamed Mwameja, Ivo Mapunda, George Masatu, Twaha Hamidu 'Noriega', Boniface Pawasa, Amri Said 'Stam', Shekhan Rashid, Athumani Machupa, Said Maulid 'SMG', Issa Manofu na wengine wengi.

Pamoja na 'Golota' kujiunga na Simba mwaka 2000, lakini umaarufu mkubwa katika klabu hiyo alianza kuupata mwaka uliofuata wa 2001, katika mchezo wa watani wa jadi, Simba dhidi ya Yanga.

Katika mchezo wa kwanza wa watani hao wa jadi Simba dhidi ya Yanga, uliochezwa katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru), Septemba 1, 2001, Simba iliibuka kwa ushindi wa bao 1-0 na bao hilo pekee lilifungwa na mshambuliaji huyo Kaniki katika dakika ya 76.

Achilia mbali mchezo huo wa kwanza dhidi ya Yanga, pia nyota huyo alionesha makeke yake katika mchezo wa marudiano, uliochezwa Septemba 30, 2001, katika Uwanja wa CCM Kirumba, mjini Mwanza.

## Tetesi za soka




MANCHESTER United wameomba kufahamishwa kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, huku winga wa Argentina Alejandro Garnacho, 20, akihusishwa na uhamisho wa kwingineko.



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.





1 SPURS pia wameonyesha nia ya kumnunua mlinzi wa Chelsea Mfaransa Axel Disasi 26, iwapo uhamisho wa mlinzi wa Uingereza Fikayo Tomori, 27, kutoka AC Milan utashindwa. (Telegraph),

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani



# Michezo Kimataifa



## TAFSIRI YA MASHABIKI KUTUPA VITU JUKWAANI

NA MWANDISHI WETU

FIKIRIA kuwa unacheza jukwaani mbele ya maelfu ya watu, na unashangaa mtu fulani katika hadhira anapokutupia kitu.

Ni kama vile kumekuwa na video inayozunguka kwenye mitandao ya kijamii kila wikendi, inayomuonesha mdau akiwarushia wasanii vitu ya ajabu na tofauti wakati wanatumbuiza.

Cardi B alikua nyota wa hivi karibuni zaidi kuvuma wakati mtazamaji alipommwagia kinywaji chake wakati wa tamasha lake la Las Vegas.

Lakini rapper huyo alichukua hatua mikononi akajibu kwa kumtupa kuwarushia maikrofoni yake kutoka stejini.

Mwanaume anayetuhumiwa kwa tukio hilo alisema alidhani kitakuwa kitendo cha kuchekesha, lakini sivyo ilivyo kwa wasanii wengi.

Harry Styles alipigwa jichoni na kipande cha peremende kwenye tamasha mnamo Novemba mwaka jana, na Pink alikasirika wakati mtazamaji alipotupa mfuko wa majivu ya binadamu kwenye jukwaa.

Mwimbaji mzuri Ava Max alipigwa kofi stejini, na mtu akamtupia bangili mwimbaji Kelsey Ballerini.

Tukio la Kelsey lilimfanya mwimbaji Charlie Puth kuwasihi mashabiki kwenye Twitter, "Mtindo huu lazima ukome, ni ukosefu wa heshima na hatari sana."

Hivi kwanini baadhi ya mashabiki wanalipa pesa kwenda kuwaona wasanii, na kuwarushia vitu?!

Dkt. Lucy Bennett ni mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Cardiff akiangalia uhusiano kati ya mashabiki na waimbaji wanaowapenda.

Anasema kuwa mshikamano wa mashabiki unaweza kujenga hisia ya "mali" ndani ya jumuiya yao na kuwaruhusu "kujieleza wao ni nani".

"Lakini, nadhani kuna kitu kimeanza kubadilika hivi karibuni," aliiambia BBC Newsbeat. "Tunaona vitendo vya mashambulizi vinavyosumbua na kuharibu zaidi na zaidi kama vile kuwarushia wasanii vitu."

Anasema pia kwamba mitazamo ya watu inaweza kuwa imebadilika tangu janga la Covid "kwamba hatuwezi kuwa kwenye matamasha".

Naye Bennett anaamini kuwa baadhi ya watu hufanya hivyo kwa sababu ni vigumu kwa wasanii kuonekana kwenye mitandao ya kijamii.

Ikawa sasa kila Jumamosi nakuwa na mchumba wangu, mwenyewe napenda kumwita Bodaboda wangu.

Nilifanya kusudi kuwa nae karibu ili nianze kumpikia na kumpa matunzo ili familia yangu isione kama nimepeleka kibaka mbele yao.

Kweli mwili wa Bodaboda wangu ukafumuka, mtoto wa kiume akaanza kunawiri mpaka sasa akaonekana ana hadhi ya kutoka na mwanamke niliyesomeshwa miaka mitatu nchini Venezuela na sasa naitumikia nchi yangu nikiongoza taasisi kubwa

Baba yangu licha ya dharau zake hasa anaposikia mwanaume anataka kuigusa familia yake lakini mbele ya Bodaboda wangu alifungwa breki!

Japo waliongea wawili tu sebuleni na mimi na Mama tukiwasubiri bustanini lakini kicheko cha furaha cha baba halikujificha.

Mipango ya ndoa kubwa yakaanza siku ileile maana baba akawa kama amepgawa kila ndugu yake alimpigia siku ileile akimueleza juu ya mimi kupata mchumba anayehitaji kunioa haraka.

Lilivyokamilika hilo niliona haja ya kuanza kumshawishi Bodaboda wangu ili ikiwezekana ahamie kwangu na yule mtoto aliyetelekezewa.

Hilo alikuwa akilipinga mara kwa mara, japo nilishambadilishia maisha huyu dogo kwa kumuwekea mfanyakazi pia kufuatilia chakula chake.

Nilitamani mtoto huyo tuanze kumleta pamoja huku na sisi tukitafuta wa kwetu baada ya harusi.


Mungu akaitikia kila kitu na siku ya harusi ikapangwa mbali kidogo, maana baba alitaka kwanza Bodaboda wangu azoee kazini maana ni kama wiki mbili hivi alikuwa amemtafutia kazi katika benki moja maeneo ya Salenda.

Ukaribu wetu na familia ya rafiki yangu msaliti Sarah ukatufanya tuungane katika maandalizi ya harusi.

Japokuwa Sarah alipata tabu mara nyingi kuniangalia usoni kutokana na kitendo chake cha kutembea na shemeji wa kwanza Martin, tena katika nyumba yangu lakini mimi nilizidisha upendo kwake ili kificha aibu ile kwa jamii.

Nilishampata mwanaume mkweli niliyemtoa barabarani akikimbiza Bodaboda, leo anakula mshahara wa benki utaniambia nini?

Hatimaye tarehe ya harusi ikapangwa na mimi sikupoteza muda, nikamtaarifu yule Mama aliyeuziwa mtoto na Sarah ili nae asikose harusini ili nijiridhishe kwa haya maajabu ninayohusi kuwa nayo kichwani. Itaendelea.



JAMVI LA HABARI
SPOTI
JUMANNE FEBRUARI 04, 2025



Aunty Ezekiel amfariji Wema Sepetu

>> Soma Uk. 15

# SIMBA YAICHOKONOA YANGA



NA MWANDISHI WETU

MASHABIKI wa Simba wanadai kuwa kikosi chao ndicho kinachocheza 'Staili' ya 'Gusa Achia' inayotumiwa na watani wao wa jadi Yanga, hivyo wamewataka wajifunze kupitia timu yao, endapo wanatamani kuona wanachokisema ndicho wanachotenda.

Hizo ni tambo za watani hao wa jadi, zilizosambaa kwa kasi mjini Tabora, wakati kikosi cha Simba kilipoivaa Tabora United na kuibuka na ushindi mnono wa mabao 3-0.

Mchezo huo ulikuwa ukifuatiliwa kwa karibu na mashabiki wa pande hizi mbili, ambapo Yanga walitamani kuona mtani wao akipoteza mechi hiyo ili wafanane na matokeo waliyokumbana nao hao katika mechi ya Ligi Kuu mzunguko wa kwanza ambapo Tabora United iliwachapwa mabao 3-1.

Hata hivyo simba ilionyesha kuukamia mchezo huo ikipeleka idadi kubwa ya mnashabiki kutoka Jijini Dar es Salaam, akiwemo Mdhamini Mkuu wa zamani wa klabu hiyo Azim Dewji ili kuhakikisha wanaondoka na Pointi zote tatu.

Baada ya kumalizika kwa mchezo huo mashabiki wa Simba wakijivunia ushindi huo, walianza kuwatambia wenzao wa Yanga waliokuwemo uwanjani humo, wakidai kuwa timu yao ndiyo iliyoonyesha staili yao ya 'Gusa Achia' tofauti na hao wenyewe walioibuni.

## Yanga yasubiri point tatu kutoka Simba

NA MWANDISHI WETU

KLABU mahasimu wa soka la Bongo Simba na Yanga, wamemaliza wikiendi yao vizuri kwa kila moja kupata ushindi mnono uliozidi kuwaimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu ya NBC.

Ilianza Yanga iliyovuna ushindi wa mabao 4-0 ikiichapa bila huruma Kagera Sugar, mchezo uliopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa KMC Mwenge Jijini Dar es salaam.

Mabao ya Yanga yalifungwa na mshambuliaji Clement Mzize dakika ya 32, kiungo Mudathir Yahya dakika ya 60, kiungo, Pacome Zouzoua kwa



Penalti kunako dakika ya 78 na mshambuliaji Mzambia, Kennedy Musonda aliyefunga dakika ya 86, kwa kichwa.

Jumapili ikawa zamu ya Wekundu wa Msimbazi ambao nao walikamilisha Kalamu yao wakiishindilia Tabora United jumla ya mabao 3-0, wakifanya mauaji hayo nyumbani kwao, Uwanja Ali hassan Mwinyi.

Mabao ya Simba mawili yalifungwa na Lionel Ateba pamoja na Shomari kapombe aliyepigilia msumari wa mwisho.

Lakini pamoja na matokeo ya Simba yaliyowafanya warejee kileleni wakiwazidi watani wao wa jadi kwa Pointii 1, Simba ikifikisha 43 na Yanga 42.



## Joseph kaniki 'golota' Mpachika mabao aluyeacha historisa Simba

**UKIWAULIZA** wanachama na mashabiki wa Simba, kuwa miaka ya 2000 mwanzoni ni mpachikaji mabao gani wa timu yao aliyekuwa na mashuti makali, ni dhairi watakuambia kuwa ni Joseph Kaniki au 'Golota'.

>> Inaendelea Uk. 15

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM